JINA: ……………………………………………………………………………………… KIDATO: …………………. NAMBARI: ………………….

102/1

KISWAHILI INSHA

KARATASI YA KWANZA

KIDATO CHA TATU

MTIHANI WA MUHULA 2

JULAI/AGOSTI 2025

MUDA: SAA 1¾

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1. Andika insha mbili .
2. Insha ya kwanza ni ya lazima.
3. Insha ya pili ichanguliwe kitoka maswali yaliyosalia.
4. Kila insha ni alama 20.
5. Maswali yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Sehemu hii imehifadhiwa kwamatumizi ya mtahini pekee.

| SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 |
|---|---|---|---|---|
| UPEO | 20 | 20 | 20 | 20 |
| ALAMA | | | | |

JUMLA

| | |
|---|---|
| UPEO | |
| ALAMA ZA MTAHINIWA | |

KARATASI HII INA KURASA MBILI ZILIZOPIGWA CHAPA. MTAHINIWA AHAKIKISHE KUWA KURASA ZOTE ZIMEPIGWA CHAPA NA MASWALI YOTE YAMO.

Enovate.co.ke

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

1. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Mzalendo, ukipendekeza njia za kupigana na uhalifu katika nchi ya Matuo. (alama 20)

**i) Swali la kwanza ni barua kwa mhariri.**
**ii) Insha iwe na sura ya barua rasmi.**
**iii) Iwe na anwani mbili (i) Anwani ya mwandishi na**
**(ii) Anwani ya mhariri wa gazeti la mzalendo.**
**iv) Mwanafunzi azingatie jina la gazeti la mzalendo.**
**v) Sehemu ya mwili izingatie njia za kupigana na uhalifu.**
**vi) Insha iwe na hitimisho – sahihi.**

**<u>Hoja za njia za kupigana na uhalifu.</u>**

- **Hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahalifu.**
- **Kuongeza askari kwani idadi yao ni ndogo ilikinganishwa na raia.**
- **Kuunda vikundi vya kujilinda.**
- **Vituo vya thamani kuwekwa mahali salama k.v benki.**
- **Kutotembea nyakati za usiku.**
- **Kujiepusha na mahali kusikofaa kama vile vichochoroni.**
- **Kuweka ua na lango makazini na kazini.**
- **Kutoa ushauri nasaha kwa wale wanaojihusisha na uhalifu.**
- **Kuongeza nafasi za ajira.**

*Mwanafunzi azingatie hoja zozote saba*

2. Jadili hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na njaa nchini. (alama 20)

**Hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na njaa nchini.**

1. **Hili ni swali la mjadala.**
2. **Mwanafunzi ajadili hoja za kupambana na njaa.**

**<u>Hoja</u>**

**i) Kufanya kilimo cha kunyunyizia maji**
**ii) Kupunguza bei ya mbolea na mbegu.**
**iii) Kutumia njia bora za kuhifadhi mazao.**
**iv) Kufanya kilimo cha mimea inayokomaa haraka.**
**v) Kufuga mifugo wanaofaa eneo na idadi unayoweza kutunza.**
**vi) Kuelimisha wakulima kuhusu njia za kisasa/ kilimo bora.**
**vii) Kutayarisha mashamba mapema.**
**viii) Serikali kununua mazao ya wakulima na kuyahifadhi.**
**ix) Kutumia mbolea ya kiasili kama (samadi)**
**x) Serikali kutoa pembejeo kwa bei nafuu au mkopo usio na riba.**

*Mwanafunzi aandike hoja zozote saba.*

3. Mwenye nguvu mpishe. (alama 20)

**Hili ni swali la methali.**

**Mwanafunzi asimulie kisa kinachodhihirisha maana ya methali; kuwa usishindane na mtu aliye na nguvu/ uwezo mkubwa kukushinda.**

4. Andika insha itakayoanzia hivi: Nilijua kuwa ningefanikiwa hiyo siku ……… (alama 20)

**Hili ni swali la mdokezo. Mwanafunzi aendeleze insha. Insha ilete dhana ya kufanikiwa katika jambo fulani. Asipomaliza kwa ushindi hajazingatia toni ya swali.**

*Mwalimu ahakikishe insha ya mwanafunzi.*

Enovate.co.ke
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes